



"Mwenyezi Mungu, Aliyetakasika na Kutukuka, atawaambia watu wa Peponi: Enyi watu wa Peponi? Watasema: Labeka tumekuitikia na umetukuka, atasema: Je, mmeridhika? Watasema: Tuna nini mpaka tusiridhike hali yakuwa umetupa mambo ambayo hujampa yeyote katika viumbe wako?

Imepokelewa kutoka kwa Saidi Al-Khuduriy -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- amesema: Amesema Mtume -rehema na amani ziwe juu yake-: "Mwenyezi Mungu,

Aliyetakasika na Kutukuka, atawaambia watu wa Peponi: Enyi watu wa Peponi?
Watasema: Labeka tumekuitikia na umetukuka, atasema: Je, mmeridhika? Watasema:
Tuna nini mpaka tusiridhike hali yakuwa umetupa mambo ambayo hujampa yeyote
katika viumbe wako? Atasema: Mimi nitakupeni kilicho bora zaidi kuliko hilo, Watasema:
Ewe Mola Mlezi, ni kitu gani kilicho bora kuliko hili? Atasema: Ninawapeni radhi zangu,
wala sitowachukia baada yake milele".

[Sahih] [Wamekubaliana Bukhaariy na Muslim]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu
atawaambia watu wa Peponi wakiwa humo: Enyi watu wa Peponi, nao watamjibu kwa
kusema: Labeka, tumekuitikia Mola wetu Mlezi! na utukufu ni wako, Atasema kuwaambia: Je
mmeridhika? Watasema: Ndiyo, tumeridhika; Kwa nini tusiridhike wakati umetupa ambacho
hukumpa kiumbe wako yeyote! Atasema Mtukufu: Je, nisikupeni kilicho bora kuliko hicho?
Watasema: Ewe Mola Mlezi, na ni kitu gani kilicho bora kuliko hicho? Atasema:
Ninakuteremshieni juu yenu radhi zangu daima; na sitokukasirikieni baada yake milele.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/8343>